Vyombo Vya Muziki Na Makosa Ya Musa Kwenye Mwamba

(Instrumental Music and Moses' Transgression at the Rock)

na

Alex S. Silvester

Vyombo Vya Muziki Na Makosa Ya Musa Kwenye Mwamba

na

Alex S. Silvester

Julai 13, 2018

Vyombo Vya Muziki Na Makosa Ya Musa Kwenye Mwamba

Hivi karibuni rafiki yangu mmoja kutota katika kanisa linalotumia vikombe vingi alimpeleka mwanaye katika shule ya kujifunza biblia. Akaniambia kwamba mtoto wao ambaye amefundishwa shuleni na wao pia kwamba matumizi ya vyombo vya muziki katika ibada ni dhambi, sasa anahoji "mafundisho ya uzima" ya wazazi wake. Huu unapaswa kuwa ni wito wa mwamko kwetu sote kwamba maswala yaliyopita yatatapakaa kama tukishindwa kudundisha misingi mizuri kwa kizazi kipya na kuwasisitiza kuwa katika kizazi kilichopo, "*Kwa maana iwapasapo kuwa waalimu, maana wakati mwingi umepita, manahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa manhitaji maziwa wala si chakula kigumu.*" (Heb. 5:12). Alieyeendelea kusema kwamba mabishano yaliyoibuliwa na mtoto yaalikuwa ni: "kifungu hakisemi kwamba hutakiwi kutumia vyombo vya muziki katika Agano Jipya wakati walizitumia katika Agano la Kale. Sasa ni nini? Waisraeli walipoondoka Misri kwenda katika nchi ya ahadi ya Kanaani, mara nyingi walifuata tamaa zao za kimwili ili iweze kuathiri maamzi yao. Pamoja na wema mwingi wa Mungu juu yao, walinung'unika na kulalamika katika safari hiyo yote. Matukio mawili yalitokea yanayofanana na kunung'unika kwao, imeandikwa katika Agano la Kale. Matukio yote haya yanahusiana na Mungu kumwagiza Musa kuchota maji mwambani (Kut. 17:1-7; Hes. 20:2-13). Ulinganifu kati ya hizi unafundisha somo lenye thamani.

Mara ya kwanza Musa kuchota maji mwambani ilikuwa ni baada ya Waisraeli kutengeneza hema huko Refidimu. Walikuwa na kiu na wakawa wasumbufu kwa Musa akathani walikuwa karibu kumpiga mawe, "*Musa akamlilia BWANA akisema niwatendee nini watu hawa? Bado kidogo nao watanipiga kwa mawe.*" (Kut. 17:4). Mungu akamwambia Musa kuchukua fimbo yake, na kwenda kwenye mwamba Horebu, na kuupiga mwamba, na maji yatatoka. Musa akafanya hivyo na maji yakatoka kama Mungu alivyoahidi. Musa kupitia uwezo wa Mungu aliweza kukidhi mahitaji ya watu na kuendelea kwenda Kanaani.

Wakati mwingine ulioandikwa ni wakati Musa anachota maji mwambani alikuwa karibia miaka arobaini huko Kadeshi, katika jangwa ya Siini, "*Kisha wana wa Israeli mkutano wote wakaingia bara ya Sini, katika mwezi wa kwanza watu wakakaa Kadeshi;; Miriamu akafa huko, akazikwa huko.*" (Hes. 20:1). Wengi wa Waisraeli kutoka katika tukio la kwanza waliangamia kutokana na kutokuwa na imani katika ahadi za Mungu (Hes. 14:1). Sasa kizazi hiki kilikuwa kinafanana na kizazi kilichopita. Angalia majivuno haya: "*…tungalikufa wakati ule ndugu zetu*

walipokufa mbele za BWANA!" (Hes. 29:3). Musa na Aruni wakaanguka kifudifudi mbele za Bwana, wwakihitaji mwongozo. Mungu akamwambia Mungu kuchukua fimbo yake, na kuwakusanya watu, na anene na mwamba, "*Twaa ile fimbo ukawakusanye mkutano, wewe na Haruni ndugu yako ukauambie mwamba mbele ya macho yao utoe maji yake, nawe utawatokezea maji katika mwamba, na hivyo utawanywesha maji mkutano na wanyama wao.*" (Hes. 20:8). Musa akatwaa fimbo akawakusanya watu wakaukaribia mwamba, badaala ya kunena nao, aliupiga mwamba mara mbili, "*Musa akaitwaa hiyo fimbo kutoka mbele za BWANA kama alivyomwamuru. Musa na Haruni wakawakusanya kusanyiko mbele ya mwamba, akawaambia sikieni sasa enyi waasi, je tuwatokezee maji katika mwamba huu? Musa akainua mkono wake akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake mara mbili maji yakatoka mengi; mkutano wakanywa naa wanyama wao pia.*"(Hes. 20:9-11). Hakufanya kama alivyoagizwa na Bwana. hata ivyo maji yalitoka, Bwana hakuacha kosa lake. Musa hakuruhusiwa kuwaongoza Waisraeli kwenda katika nchi ya ahadi kwa sababu ya kosa lake. Musa aliruhusiwa kuangalia nchi yaa Kaanani kutoka katika mlima wa Nebo, na alikufa akiwa katika nchi ya Wamoabu, (Kumb.32:48-52;34:1).

Matukio haya mawili yanahusiana vipi na vyombo vya musiki? Wengine kwa kupenda vyombo vya muziki wanauliza, "Ni wapi Agano Jipya linasema hupaswi kuabudu kwa kutumia vyombo vya muziki katika kumwabudu Mungu?" Swali siyo "Ni wapi Agano Jipya linasema huwezi kumwabudu Mungu kwa vyombo?" Badala yake, swali ni: Agano Jipya linaruhusu wapi kuabudu kwa kutumia vyombo? Tukio la kwenye mwamba linaeleza somo lenye thamani kwamba tunatakiwa kufuata mapenzi ya Mungu kama alivyo yaagiza na wakati aliouruhusu. Moja ya ubishi unaotumiwa na watumiaji wa vyombo vya muziki ni "Matumizi ya vyombo vya muziki katika kumwabudu Mungu katika Agano la Kale; hivyo basi, Mungu hajali kwa hakika tutumie au tusitumie vyombo leo." Mtu anatakiwa kusoma mamlaka ya Biblia kwa karibu. Paulo aliandika: "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, huku ukilitumia kwa halali neno la kweli.*" (2 Tim. 2:15). Tunapaswa kufahamu kwamba Mungu alibadilisha maelekezo katika mwamba wa pili kutoka wakati Musa alipoleta maji kutoka katika mwamba wa kwanza. Siyo tu kwamba Mungu hakuona kosa la Musa kutoka katika maelekezo yake mapya. Musa aliadhibiwa kwa kukosa utii.

Kama Musa alikosa nchi ya ahadi ya Kanaani kwa sababu alifuata maelekezo ya zamani badala ya njia mpya ambayo Mungu alimpa, sasa itakuwaje hali zao wale wanafanya filosofia inayosema "Vyombo vya muziki inaweza isiwe katika Agano Jipya lakini iko katika Agano la Kale." Mungu alitoa maelekezo ya wazi aliyotarajiwa kufuatwa. Unaweza

kuona kwamba maji ya kwanza yalikuwa kabla ya sheria ya Musa, lakini ya pili ilikuwa wakati wa sheria ya Musa. Mungu alimhesabia Musa makosa kwa maelekezo yake mapya hataivyo miaka michache imepita toka katika maelekezo ya awali. Chini ya miaka arobaini imepita toka katika badiliko la maagizo ya Mungu kwa Musa, lakini miaka mamia imepita kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Kwa nini watu hawani kwamba wanatakiwa kutumia sheria waliopewa katika Agani Jipya na wasiangalie nyuma katika matendo ya ibada katika Agano Jipya?

Makanisa ya Kristo yameonyesha toka zamani kwamba matumizi ya vyombo vya muziki katika ibada ni dhambi. Hata katika kuimba, kila Agano Jipya linalohusu muziki kanisani inasema "*imba*"; kama vile, "*Mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu;*" (Efe. 5:19). Haisemi, "piga makofi", "piga ngoma", "piga kinanda", au chochote kinachofanana na hayo yaliyotengenezwa na wanadamu. Ni dhambi ya kusudi kudhani kwamba tunaweza kufanya jambo lingine tofauti na "*kuimba*". Tunaambiwa katika Zaburi 19:13, "*Umzuie mtumishi wako asitende mambo ya kiburi, yasinitawale mimi. Ndipo nitakapokuwa kamili, nami nitakuwa safi, sina kosa lililo kubwa.*" Wapo wale wanaodai kwamba, "Ndio, lakini Daudi alipiga vyombo vya muziki!" Ndiyo alipiga, lakini je Mungu alipendezwa naye? Hakika Mungu hakupendezwa: "***Ole wao wanaostarehe katika Sayuni, na hao wanaokaa salama katika mlima wa Samaria, watu mashuhuri wa taifa lililo la kwanza, ambao nyumba ya Israeli huwaendea. Ninyi mnaoimba nyimbo za upuzi pamoja na sauti ya vinanda, na kujifanyizia vinanda vya namna nyingi, kama vile Daudi.*" (Amosi 6:1, 5).** Hatuwezi kumtumia Daudi kama mfano wa kutumia vyombo vya muziki.

Kwa hili naongea kuhusu wale wanaoabudu kulingana na maagizo ya Mungu alioyatoa katika Agano Jipya. Ni dhambi kwa sababu iyo hiyo ambayo Mungu zalitenda dhambi katika mwamba wa pili, kwa sababu maelekezo ya Mungu yamebadilika na Musa alishindwa kutii amaagizo mapya.